# Jarida Maalum la Shirika la Posta Tanzania




Toleo Maaalum | Januari 2022

www.posta.co.tz

# BODI YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**
Macrice D. Mbodo
Kaimu Postamasta Mkuu,Shirika la Posta Tanzania

**MRATIBU NA MHARIRI WA JARIDA**
Elia P. Madulesi
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano,Shirika la Posta Tanzania

**MUANDAAJI/MSANIFU WA JARIDA**
Loema Joseph

**WAHARIRI**
Mashala Lufunga
Jane Sallu & Rachel Kitinya



# 01 POSTA TUMIENI ANWANI ZA MAKAZI KUBUNI HUDUMA MPYA KWA WATEJA.

Serikali imelitaka Shirika la Posta Tanzania (TPC) kutumia mfumo wa anwani za makazi na postikodi kubuni huduma mpya kwa wateja ili utekelezaji wa mfumo huo utakapokamilika uweze kutumika ipasavyo kufikisha huduma na bidhaa kwa wateja.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Teddy Njau wakati akifungua semina ya mafunzo ya kujenga uelewa kuhusu mfumo wa anwani za makazi na postikodi kwa Mameneja wa Mikoa ya Shirika hilo wa Tanzania Bara na Zanzibar.

Njau amewataka washiriki hao kuweka anwani za makazi kwenye maeneo yao; kwa wateja wao na kubuni huduma mpya zitakazotumiwa na wateja kupitia mfumo wa anwani za makazi utakapokamilika utekelezaji wake kwa kuwa Shirika hilo lina mtandao mpana nchi zima na ni wadau wa msingi wanaotakiwa kutumia miundombinu hiyo.

“Kila mmoja wetu ana jukumu la kuhakikisha anwani za makazi zinawekwa na kutumika nchi nzima, leo mnapatiwa mafunzo ya kujenga uelewa ili mkasimamie na kushiriki utekelezaji wa mfumo huu kwenye mikoa yenu Tanzania Bara na Zanzibar kwa kuwa ninyi ni wadau muhimu na ni wajumbe kwenye kamati za kitaalam,” amesisitiza Njau.




# Wadi 4,174, Halmashauri 196 na Mikoa 31 Nchini kunufaika na Mfumo wa Anwani za Makazi.

Akizungumza kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi kufungua mafunzo hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Mawasiliano wa Wizara hiyo, Caroline Kanuti amesema kuwa mfumo wa anwani za makazi utakuwa wa kidijitali ili kutoa fursa kwa Serikali kutekeleza majukumu ya sensa ya watu na makazi ili anwani zijumuishwe kwenye sensa inayoanza mwezi Agosti mwaka huu.

Ameongeza kuwa utekelezaji wa mfumo wa anwani za makazi utafanyika kwa miezi mitano nchi nzima kwenye kata na wadi 4,174; halmashauri 196 na mikoa 31 ili zoezi hili likamilike ipasavyo na taarifa zake ziwekwe kwenye tovuti maalum na zitumike kwenye simu za mkononi ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Naye Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika hilo, Macrice Mbodo amesema kuwa Shirika lake ni mdau muhimu katika anwani za makazi na postikodi ndani na nje ya nchi kwa kuwa posta zote duniani zina jukumu la kutoa anwani zinazotambulika na muundombinu huu utakapokamilika Shirika litatumia anwani za makazi kusafirisha huduma na bidhaa kwa wananchi mpaka nyumbani kwa kuwa tayari tuna duka mtandao.

"Mwananchi anaweza kununua na kuuza huduma au bidhaa na kuweka anwani yake kisha atasafirishiwa mzigo wake mpaka mahali alipo na mwananchi atatumia muda wake kutekeleza majukumu mengine ya kiuchumi na kijamii badala ya kufuata mzigo wake, tutashirikiana na viongozi na wataalam wengine nchi nzima kutekeleza hili," amesema Mbodo.

Amesititiza kuwa Shirika lina duka mtandao ambalo linamuwezesha mwananchi wa ndani na nje ya nchi kufanya biashara mtandao na kutumia huduma za Shirika hilo kwa kuwa limeunganishwa na mtandao wa ofisi nyingine za Posta 670 duniani zilizopo kwenye nchi 192 wanachama wa Umoja wa Posta Duniani (UPU) ambapo Tanzania ni nchi mwanachama.



# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI.




Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Teddy Njau akizungumza wakati akifungua rasmi semina ya kujenga uelewa kwa viongozi na watendaji wa Shirika la Posta Tanzania katika ukumbi wa VETA, jijini Dodoma.




Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Mawasiliano, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Caroline Kanuti akizungumza wakati wa ufunguzi rasmi wa semina ya kujenga uelewa kwa viongozi na watendaji wa Shirika la Posta Tanzania iliyofunguliwa na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Teddy Njau katika ukumbi wa VETA, jijini Dodoma.



Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Macrice Mbodo akizungumza wakati wa ufunguzi rasmi wa semina ya kujenga uelewa kwa viongozi na watendaji wa Shirika la Posta Tanzania iliyofunguliwa na Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Teddy Njau katika ukumbi wa VETA, jijini Dodoma.



# 02 SHIRIKA LA POSTA TANZANIA LAFANYA MAZUNGUMZO NA IDARA YA FEDHA MAMLAKA YA MAWASILIANO MALAWI.

## Huduma ya Posta Kiganjani na Duka Mtandao zawavutia mataifa ya Jirani.”

Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Constantine Kasese kwa niaba ya Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika hilo Bw. Macrice Mbodo amekutana na kufanya mazungumzo na Meneja wa Fedha wa Mfuko wa Mawasiliano Mamlaka ya Mawasiliano Malawi, Bi. Limba Mkandawire katika ofisi za Shirika hilo, jijini Dodoma, tarehe 27 Januari, 2022.

Lengo la ziara ya Bi. Limba ni kufahamu shughuli zinazofanywa na Shirika la Posta nchini katika kufikisha huduma zake kwa jamii hasa katika kuendana na mabadiliko ya Teknolojia yanayoendelea duniani, ambapo ameweza kufahamu huduma za kidijitali zilizoanzishwa na Shirika la Posta ikiwemo Huduma ya Duka Mtandao na Posta Kiganjani.

Ziara hiyo imehudhuriwa na Baadhi ya watendaji wa Mfuko wa Mawasiliano UCSAF akiwemo Mkuu wa Idara ya Fedha na Utawala wa UCSAF pamoja na baadhi ya watendaji kutoka Shirika la Posta.



# 03 SERIKALI KUENDELEA KUWEKA MAZINGIRA WEZESHI KWA SHIRIKA LA POSTA TANZANIA

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imeahidi kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Shirika la Posta nchini lengo ikiwa ni kuongeza uzalishaji na kutekeleza majukumu yake ili kuendana na lengo la uanzishwaji wa Shirika kwa mujibu wa Sheria iliyounda Shirika hilo.

Hayo yameelezwa leo tarehe 28 Januari, 2022 na Msajili wa Hazina Ndg. Mgonya Benedicto wakati akifunga mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania katika ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Convention Center, jijini Dodoma.

Ndg. Mgonya amesema kuwa Serikali inatambua mchango wa Shirika la Posta katika kuwahudumia wananchi hasa katika sekta ya Mawasiliano ndiyo maana inaendelea kuliongezea nguvu Shirika ili liendelee kutoa huduma stahiki na zinazoendana na mahitaji ya wakati ya wananchi.

Itakumbukwa kuwa mwaka jana, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iliamua kulipunguzia mzigo Shirika wa kuwalipa wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki baada ya Serikali kuchukua jukumu hilo na pia Serikali ililirejeshea Shirika kiasi cha Bilioni 7.9 ikiwa ni fedha lilizotumia kuwalipa wastaafu hao kwa kipindi Cha kuanzia mwaka 1994 2006 na 2015-2020 lengo likiwa ni kuliongezea ufanisi Shirika hilo.

"Serikali iliamua kurejesha Tshs. 7.9 bilioni ikiwa ni fedha walizolipwa wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki ili kuweka mazingira wezeshi kwa Shirika kuongeza uzalishaji na kutekeleza majukumu yake". Amesema Mgonya.

Aidha Msajili wa Hazina amelitaka Shirika la Posta kuzitumia fedha hizo kwa kuzingatia maelekezo na malengo ya fedha hizo katika kuboresha vitendea kazi vya Shirika, pia amewataka watendaji wa Shirika hilo kuongeza ubunifu ili kuleta tija katika kuongeza pato la Taifa na hatimaye kuweza kutoa gawio kwa Serikali.

Sambamba na hilo, Ndg. Mgonya ameahidi Ofisi yake itaendelea kushirikiana na Shirika katika utatuzi wa changamoto za kiuendeshaji na kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa kushirikiana na Serikali ikiwemo suala la Mtaji kwa Shirika na malimbikizo ya madeni ya kodi ya muda mrefu (ya shilingi Bilioni 26 yanayotakiwa kuchukuliwa na Serikali).

Akizungumza wakati akimkaribisha Msajili wa Hazina, Mkurugenzi Msaidizi Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Bwana Elisa Mbise kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo amesema kuwa, Serikali iko tayari kuliboresha Shirika la Posta ili liongeze tija kwa Taifa na kuwataka watendaji wa Shirika kuonesha uwezo wa kutumia rasilimali walizonazo ili Serikali iendelee kuona umuhimu wa kuliimarisha Shirika hilo kiutendaji.

"Oneshení uwezo wa kutumia rasilimali mlizonazo ili Serikali ione umuhimu wa kuendelea kuwaongezea mtaji muweze kuboresha utendaji wenu ili wananchi waendelee kunufaika na huduma za Posta". Alisema Mbise.

Naye Kaimu Postamasta Mkuu wa TPC, Bwana Macrice Mbodo amesema kuwa katika mkutano huo, wajumbe wamepatiwa mafunzo ya huduma kwa mteja; wamepitia Mpango Mkakati mpya wa miaka mitano (2022/33 – 2025/26) unaojikita kuifanya Posta ya Kidijitali kwa maendeleo endelevu pamoja na kupitia Mapendekezo ya Mpango Mkakati mpya wa nane wa kibiashara wa miaka mitano (2022/23 - 2026/27).

Akitoa salamu za shukrani kwa niaba ya Baraza Afisa Masoko Mwandamizi kutoka Zanzibar Bi Halima Abdulla Hamad amemshukuru Msajili wa Hazina kwa kutenga muda wake kufunga Baraza hilo, na kuahidi kutekeleza yote waliyoyajadili katika kikao hicho ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Shirika.

Mkutano huo umehudhuriwa na Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi), Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi kitaifa wa Bara na Zanzibar pamoja na Viongozi wa Shirika la Posta kwa ngazi ya Makao Makuu na Mikoa.

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI.




Msajili wa Hazina Mgonya Benedicto akizungumza wakati akifunga rasmi Mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania katika ukumbi wa Jakaya kikwete Convention Center jijini Dodoma.




Mkurugenzi Msaidizi Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Bwana Elisa Mbise kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo akizungumza wakati wa kufunga rasmi Mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania uliofungwa rasmi na Msajili wa Hazina Mgonya Benedicto, katika ukumbi wa Jakaya kikwete Convention Center jijini Dodoma.




Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Macrice Mbodo akizungumza wakati wa kufunga Mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika hilo uliofungwa rasmi na Msajili wa Hazina Mgonya Benedicto, katika ukumbi wa Jakaya kikwete Convention Center jijini Dodoma.

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI.



Baadhi ya wajumbe wa Mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania wakifuatilia mkutano huo uliofungwa rasmi na Msajili wa Hazina Mgonya Benedicto (hayupo pichani), katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Center, jijini Dodoma.




Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Macrice Mbodo (kulia) akimkabidhi zawadi Msajili wa Hazina Mgonya Benedicto mara baada ya kufunga rasmi Mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika hilo, katika ukumbi wa Jakaya kikwete Convention Center jijini Dodoma.

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI.



Msajili wa Hazina Mgonya Benedicto (kushoto) akiteta jambo na Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Macrice Mbodo kabla hajafunga rasmi Mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika hilo, katika ukumbi wa Jakaya kikwete Convention Center jijini Dodoma.



Msajili wa Hazina Mgonya Benedicto (katikati) akiwasili kwa ajili ya kufunga rasmi Mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre jijini Dodoma. Kushoto ni Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika hilo Macrice Mbodo na kulia ni Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara wa Shirika hilo Constantine Kasese




# 04 SERIKALI KUENDELEA KUBORESHA HUDUMA ZA POSTA NCHINI

Naibu Waziri wa Habari,Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Mhandisi Kundo Mathew ametaka wadau wa Sekta ya Posta nchini kushirikiana katika kuhakikisha utoaji wa huduma zenye tija kwa wananchi.

Hayo ameyasema tarehe 18 Januari, 2022, alipokuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya Siku ya Posta Afrika (PAPU) ambapo amemwakilisha Waziri wa Habari,Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye.

Mhe. Kundo amesema kuwa Serikali inatambua juhudi ambazo Sekta ya Posta nchini inafanya katika kuendana na maendeleo ya teknolojia ambayo yamekuwa chachu ya kubadili mifumo mbalimbali ya kiutendaji ndani ya Shirika la Posta.

"Serikali inatambua juhudi ambazo Sekta ya Posta inafanya kuelekea mageuzi yanayoletwa na teknolojia na kubadili mifumo mbalimbali ya kiutendaji ndani ya Shirika la Posta". Alisema Mhe. Kundo.

Aidha, Mhe. Kundo ameongeza kuwa, Tanzania imepiga hatua kubwa katika utoaji wa huduma za posta na kituo Cha kutegemeza TEHAMA kwa nchi zinazoongea kiingereza kipo nchini Tanzania hivyo uwepo wa Makao Makuu ya Umoja wa Posta (PAPU) Jijini Arusha unaimairisha umuhimu wa ufanisi wa utoaji huduma za posta katika nchi mbalimbali.

Kwa upande wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Posta Afrika, Chief Sifundo Moyo alisema Umoja huo unazidi kukua kwa kuboresha huduma mbalimbali za posta ikiwemo kushirikishana mbinu za mashirika ya posta kutokana na ukuaji wa teknolojia hususan teknolojia za simu na usafirishaji wa mizigo kupitia posta cargo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Dkt. Jabiri Bakari amesema, TCRA itaendelea kusimamia na kuunga mkono jitihada za Sekta ya Posta nchini katika kukuza mawasiliano yatakayoleta tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Naye PostaMasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania,Macrice Mbodo amesema kuwa katika mkakati wa nane Shirika hilo limeweka vipaumbele katika huduma za usafirishaji, huduma za fedha na uwakala, biashara mtandao, uimarishaji wa vituo vya Huduma Pamoja na mifumo ya TEHAMA .

Nao wadau wa Posta wameiomba Serikali kuondoa mkanganyiko wa ushuru wa forodha ambao umekuwa ukisababisha wafanyabishara kutoingiza bidhaa zao nchini na badala yake kutumia nchi ya Kenya kuingiza mizigo na kuisafirisha kuja nchini kwa njia ya biashara mtandao kwani kutokana na ushuru wa forodha kutoeleweka katika bidhaa wanazoagiza nje ya nchi kuja nchini kampuni mbalimbali za usafirishaji zinashindwa kuelewana na wateja na hatimaye wateja kususia mizigo yao na kampuni kupata hasara.

Maadhimisho hayo yenye kauli mbiu **"Kuimarisha Ushirikiano na Watoa Huduma Wengine wa Sekta ya Posta Afrika"** yalihudhuriwa na Viongozi mbalimbali akiwemo Katibu Mkuu wa Umoja wa Posta Afrika (PAPU) Bwana Sifundo Chief Moyo na Msaidizi wake Bibi Jessica Hope Ssengooba, Mkuu wa Wilaya ya Arusha Mjini Mhe. Said Mtanda aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA Dkt. Jabir Bakari, Mtendaji Mkuu wa UCSAF Bibi Justina Mashiba, Katibu Mtendaji wa TCRA CCC Bibi Mary Msuya, Mkurugenzi wa TEHAMA kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari aliyemwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara Dkt Jim Yonazi na wadau mbalimbali wa Sekta za Mawasiliano nchini, ikiwemo Chama Cha watoa huduma za Posta nchini.



Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Mhandisi Kundo Andrea Mathew akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Posta Afrika, tarehe 18 Januari, 2022, jijini Arusha.







Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Mhandisi Kundo Andrea Mathew (kulia) akifurahia jambo na Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo (kushoto) wakati alipotembelea banda la Shirika la Posta wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Posta Afrika, tarehe 18 Januari, 2022, jijini Arusha.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Posta Afrika Bw. Sifundo Chief Moyo akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Posta Afrika, tarehe 18 Januari, 2022, jijini Arusha.







Washiriki wa Maadhimisho ya Siku ya Posta Afrika wakiwa na mabango yenye kauli mbiu ya maadhimisho ya Siku ya Posta Afrika wakati wa maandamano yaliombatana na maadhimisho hayo, tarehe 18 Januari, 2022, jijini Arusha.



# 05 POSTA MUWE KINARA UTEKELEZAJI WA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI NCHI NZIMA

Serikali imelielekeza Shirika la Posta Tanzania (TPC) kuwa kinara na kuongoza jukumu la utekelezaji wa mfumo wa anwani za makazi na postikodi linaloendelea nchi nzima, Hayo yameelezwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape Nnauye wakati akifungua rasmi Mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika hilo uliofanyika kwenye ukumbi wa Jakaya Kikwete, Dodoma leo.

Waziri Nape amesema kuwa utekelezaji wa mfumo wa anwani za makazi na postikodi utafanikisha na kuwezesha Posta ya Kidijitali na utendaji wa Shirika katika kuhudumia wateja na wananchi kwa ujumla na amewataka Mameneja wote wa TPC kushiriki kikamilifu katika jambo hili la anwani za makazi.

"Mameneja wa Mikoa yote wa Shirika la Posta Tanzania muwe wajumbe maalum na wa kudumu kwenye kamati ya utekelezaji wa mfumo wa anwani za makazi na postikodi nchi nzima na muongoze utekelezaji wa jambo hili mikoa yote nchi nzima", amesititiza Waziri Nape.

Amewataka wajumbe wa Baraza la 28 la Mkutano huo kujadili kwa uwazi, kuambizana ukweli na kukosoana kwa staha ili kujenga umoja, kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa kuwa anatambua kuwa uhai wa Shirika umebebwa na wafanyakazi wenyewe na Wizara itawasiliana na Wizara ya Fedha ya Mipango ili kufanikisha malipo ya deni la shilingi bilioni 26 kwa lengo la kuliondolea mzigo Shirika.

Akizungumza wakati akimkaribisha Waziri Nape, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt. Jim Yonazi amesema kuwa wateja wanataka kuona TPC ya kisasa inayofanana na mashirika mengine duniani na tayari TPC imeonesha taswira hii na Shirika linakua kiuchumi.

"Wateja wetu cha kwanza anachokutana nacho siyo huduma unayompatia bali unavyompokea na kumhudumia, hivyo tuhudumie wateja wetu vizuri, tuipeleke mbele Serikali kwa kuwa tunawakilisha Serikali na tunafanya kazi kwa niaba ya Serikali," amesisitiza Dkt. Yonazi.

Naye Kaimu Postamasta Mkuu wa TPC, Macrice Mbodo amesema kuwa katika mkutano huo, wajumbe watapatiwa mafunzo ya huduma kwa mteja; kupitia Mpango Mkakati mpya wa miaka mitano (2022/33 – 2025/26) unaojikita kuifanya Posta ya Kidijitali kwa maendeleo endelevu; na kupitia bajeti na majukumu ya Shirika hilo kwa mwaka 2022/23.

Akitoa salamu za shukrani kwa niaba ya wengine, Meneja wa TPC wa Mkoa wa Dodoma, Ferdinand Kabyemela amemshukuru Waziri Nape kwa kuwatengeneza, wataishi kwa upendo ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa kuwa wana rubani na kapteni mzuri Mbodo anayewaongoza vema kutekeleza majukumu ya Shirika.

Pia, mkutano huo umehudhuriwa na Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi), Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage; Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Justina Mashiba; na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Samson Mwela.





Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye akizungumza wakati akifungua rasmi Mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania katika ukumbi wa Jakaya kikwete Convention Center jijini Dodoma.



Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Macrice Mbodo (wa pili kulia) akimkabidhi zawadi Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye mara baada ya kufungua Mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika hilo katika ukumbi wa Jakaya kikwete Convention Center jijini Dodoma.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye (kulia) akiteta jambo na Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Macrice Mbodo kabla hajafungua rasmi Mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika hilo, uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya kikwete Convention Center jijini Dodoma.




# 06 SHIRIKA LA POSTA LAPOKEA UGENI WA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar leo tarehe 21 Januari imelitembelea Shirika la Posta Tanzania (TPC) ili kujionea utendaji na huduma mbalimbali zinazotolewa na Shirika hilo.

Kamati hiyo ilianza ziara hiyo kwa kupokea kupokea taarifa ya utendaji ya Shirika hilo ikiangazia historia ya kuanzishwa kwake, mapito mbalimbali lililopitia Shirika tangu kuazishwa kwake mwaka 1994 hadi sasa. Pia mwelekeo wa sasa wa Shirika katika kutoa huduma zake.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo Bwana Yahya Rashid amesema wamefurahishwa na utendaji kazi wa Shirika la Posta Tanzania hususan ni namna lilivyojipanga kwenye kuhakikisha wananchi wanapata huduma zenye tija kulingana na mahitaji yao ya sasa.

Aidha, Mwenyekiti wa Kamati hiyo Yahya Rashid amelipongeza Shirika la Posta nchini kwa kuendelea kukuza na kuimarisha uhusiano kati yake na Taasisi mbalimbali zilizopo visiwani Zanzibar kwani ushirikiano huo utaboresha zaidi upatikani wa huduma mbalimbali kwa pande zote za Muungano wa Tanzania.

“Napongeza ushirikiano uliopo kati ya Serikali zetu za Tanzania Bara na Zanzibar kupitia Taasisi zetu hizi kwani kutaleta huduma bora kwa wananchi wetu”. Alisema Yahya

Katika hatua nyingine, Bw. Yahya amelitaka Shirika la Posta kuhakikisha linatoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi sahihi ya huduma za Posta nchini kwani wananchi wanapaswa kufahamu na kutumia huduma za Posta za kisasa za kidijitali.

"Wananchi wanahitaji kuelimishwa kuhusu huduma za Posta, mkawajengee uelewa wa kutosha kwa sababu Shirika la Posta lina fursa za kibiashara na kuna huduma za kidigitali na gharama zake ni nafuu na ni za uhakika". Amesema Yahya.

Kwa upande wa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali aliyeambatana na msafara wa Kamati hiyo amesema kufika kwao kama Wizara katika Shirika la Posta kumesaidia kufahamu masuala mbalimbali ambapo hawakuwa na uelewa nayo na kupata elimu na ufahamu wa mambo mengi ya msingi na yenye manufaa kwa jamii ya watanzania.

"Nimefarijika sana kufika hapa leo, nimepata nafasi ya kujifunza na kufahamu namna Shirika la Posta linavyofanya kazi zake kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar, hii itatusaidia sana kwenye mambo mengi tunaosimamia sekta ya mawasiliano". Amesema Mhe. Rahma.

Aidha, Mhe. Waziri ameahidi kuwa, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara yake itaendelea kutoa ushirikiano kwa Shirika la Posta nchini ili kuhakikisha wananchi wa pande zote za Muungano wanapata huduma bora na zenye tija kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla.

Naye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye (Mb) ameishukuru na kuipongeza Serikali ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuona umuhimu wa kufika Makao Makuu ya Shirika la Posta nchini na kujionea shughuli mbalimbali pamoja na huduma zinazotolewa na Shirika hilo. Pia ameahidi kuendelea kutoa ushirikiano katika kuhakikisha wananchi wa pande zote za Muungano wananufaika na huduma za Posta.

Naye, Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo ameishukuru Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa kutenga muda wao na kuja kulitembelea Shirika la Posta . Kaimu Postamasta Mkuu ameongeza kuwa, zipo fursa mbalimbali ambazo Shirika la Posta linazifanyia kazi kwa upande wa Zanzibar ikiwemo Duka Mtandao ambalo linawawezesha wananchi kuuza na kununua bidhaa zao katika duka hilo na kufikishwa popote walipo. Pia fursa ya huduma za usafirishaji ambapo mwananchi ataweza kufikishiwa bidhaa na huduma mahali popote alipo kupitia mfumo wa anuani za Makazi na Postikodi unaoendelea kujengwa hapa nchini kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Katika hatua nyingine, Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar pamoja na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali walipata wasaa ya kutembelea Kituo cha Huduma Pamoja kinachotoa huduma mbalimbali za kiserikali, kilichopo katika Ofisi kuu ya Mkoa wa Dar es Salaam na kujionea huduma mbalimbali zinazotolewa katika kituo hicho.

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI




Mwenyekiti wa Kamati Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar Bwana Yahya Rashid (kushoto) akizungumza wakati wa kikao cha Kamati hiyo na Shirika la Posta Tanzania, katika Makao Makuu ya Shirika hilo, tarehe 21 Januari, 2022, jijini Dar es Salaam.




Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali (kulia) akizungumza wakati wa kikao cha Kamati Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Shirika la Posta Tanzania, katika Makao Makuu ya Shirika hilo, tarehe 21 Januari, 2022, jijini Dar es Salaam.




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye akizungumza wakati wa kikao cha Kamati Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Shirika la Posta Tanzania, katika Makao Makuu ya Shirika hilo, tarehe 21 Januari, 2022, jijini Dar es Salaam.



Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara za Shirika la Posta Tanzania Bw. Constantine Kasese akitoa wasilisho kuhusiana na historia ya Shirika hilo wakati wa kikao cha Kamati Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Shirika hilo, katika Makao Makuu ya Shirika la Posta, tarehe 21 Januari, 2022, jijini Dar es Salaam.

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye (kushoto) akiteta jambo na Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo wakati wa kikao cha Kamati Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Shirika hilo, katika Makao Makuu ya Shirika la Posta, tarehe 21 Januari, 2022, jijini Dar es Salaam.




Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Bw. Amour Hamil Bakar akizungumza wakati wa kikao cha Kamati Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Shirika la Posta Tanzania, katika Makao Makuu ya Shirika la hilo, tarehe 21 Januari, 2022, jijini Dar es Salaam.




Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali (Kushoto) akiteta jambo na Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo wakati wa Kikao cha Kamati Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Shirika hilo, katika Makao Makuu ya Shirika la Posta, tarehe 21 Januari, 2022, jijini Dar es Salaam.

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI




Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo (kulia) akikabidhi zawadi kwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali mara baada ya kikao cha Kamati Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Shirika hilo, katika Makao Makuu ya Shirika la Posta, tarehe 21 Januari, 2022, jijini Dar es Salaam.




Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo (kulia) akikabidhi zawadi kwa Mwenyekiti wa Kamati Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar Bwana Yahya Rashid mara baada ya kikao cha Kamati hiyo na Shirika la Posta, katika Makao Makuu ya Shirika hilo, tarehe 21 Januari, 2022, jijini Dar es Salaam.



Kaimu Meneja Mkuu Rasilimali za Shirika la Posta Tanzania Bw. Aron Samwel akitoa neno la shukrani mara baada ya kikao cha Kamati Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Shirika hilo, katika Makao Makuu ya Shirika la Posta, tarehe 21 Januari, 2022, jijini Dar es Salaam.




Mwenyekiti wa Kamati Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar Bwana Yahya Rashid pamoja na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Shirika la Posta Tanzania mara baada ya kikao cha Kamati hiyo na Shirika la Posta, katika Makao Makuu ya Shirika hilo, tarehe 21 Januari, 2022, jijini Dar es Salaam.



# 07 LAZIMA MATOKEO YAONEKANE KWA KILA ANAYETUMIKA KATIKA SHIRIKA HILI - KAIMU POSTAMASTA

Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo amewataka wajumbe wa Baraza la Majadiliano wa Shirika hilo nchini kuchukua kila fursa inayoonekana inaleta tija kwa Shirika kwa lengo la kuhakikisha wanachi wanapata huduma bora na zinazoendana na mahitaji yao kulingana na mabadiliko ya Teknolojia.

"Kila kiongozi aone umuhimu wa kuchukua kila fursa kama inavyotakiwa na kuwajibika kwa nafasi yake ili kuleta tija kwa Shirika na Taifa". Alisema Mbodo

Aliyasema haya tarehe 13 Januari, 2022 wakati alipokuwa akifungua rasmi Mkutano wa Baraza la Majadiliano unaofanyika ukumbi wa mikutano wa Chuo cha Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) kampasi ya Bagamoyo huku ukihudhuriwa na viongozi wa vyama vya wafanyakazi na wawakilishi wa Menejimenti ya Shirika la Posta nchini.

Aidha, Bw. Mbodo ametumia nafasi hiyo kuwafamisha wajumbe wa Baraza hilo kuwa Serikali Kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ikishirikiana na Wizara inayosimamia Sekta ya Posta; Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari nchini imepokea mapendekezo ya mabadiliko ya muundo wa utendaji wa Shirika yenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Shirika la Posta Tanzania.

Ameendelea kueleza kuwa, muundo uliopo sasa umebana upatikanaji wa baadhi ya fusra kwa kuwa Idara na Kurugenzi zimewekewa majukumu mengi yanayosababisha kupunguza ufanisi katika kutoa huduma kwa wananchi. Hivyo maboresho ya muundo huo yatamuwezesha kila mwananchi kunufaika na huduma zinazotolewa na Shirika hili nchini.

"Muundo huu unaopendekezwa una maboresho machache ambayo yamefanywa ili kugawanya majukumu yatakayotuwezesha kuziona na kuzipata kwa urahisi fursa zilizopo sokoni kwani tukiendelea kuubana hatuwezi kuzipata fursa hizo". Alisema Mbodo

Sambamba na hilo, Bw. Mbodo amewataka wajumbe wa Baraza hilo kuhakikisha wanaleta matokeo chanya yenye lengo la kukuza mapato ya Shirika kwa kuwajibika katika nafasi zao na kufanya kazi kwa weledi na kwa ufanisi.

"Ni lazima matokeo yaonekane kwa kila aliyepewa nafasi ya kutumika katika Shirika hili ahakikishe analeta matokeo". Alisema Mbodo

Naye Mwenyekiti wa Baraza hilo Bwana Omari M. Dibibi amempongeza Kaimu Postamasta Mkuu kwa utendaji wake na amemshukuru kwa kukubali kufungua mkutano na kumuahidi kuendesha mkutano huo kwa weledi ili kuleta matokea chanya kwa Shirika kama ilivyokusudiwa.

Kwa upande wa Msemaji Mkuu wa Wafanyakazi Junus Ndaro alipongeza juhudi zilizofanyika na mikakati mizuri inayoonekana ya kuboresha utendaji wa Shirika ikiwa ni sehemu ya kuliboresha Shirika la Posta nchini kwa maslahi mapana ya taifa letu.



Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Macrice Daniel Mbodo (Kushoto) akizungumza na Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) Dkt. Siston Masanja Mgullah (kulia) mara baada ya kuwasili katika chuo hicho kwa ajili ya kufungua rasmi mkutano wa Baraza la Majadiliano wa Shirika hilo, mjini Bagamoyo.



Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Macrice Daniel Mbodo (katikati) akizungumza na Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara za Shirika la Posta Bw. Constantine Kasese (kushoto) pamoja na Kaimu Meneja Mkuu Rasilimali za Shirika Bw. Samwel Aron (kulia), mara baada ya kuwasili katika Chuo cha Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), kwa ajili ya kufungua rasmi mkutano wa Baraza la Majadiliano wa Shirika hilo, mjini Bagamoyo.



# 08 SHIRIKA LA POSTA MWANZA, LAUKARIBISHA MWAKA 2022

Tarehe 15 Januari 2022, Shirika la Posta mkoa wa Mwanza, limefanya hafla fupi ya kuukaribisha mwaka 2022 zilizoambatana na kuwaaga wastaafu wa Shirika hilo mkoani Mwanza.

Aidha katika hafla hiyo Shirika la Posta mkoani humo lilipata nafasi ya kushiriki Bonanza maalum wakishirikiana na "jogging club" za Wasafi media pamoja na EFM.

Vilevile, Wafanyakazi wa Shirika la Posta mkoa wa Mwanza walifanya ibada maalum na kutoa sadaka kwenye kituo cha watoto Yatima cha Upendo malimbe, kilichopo mkoani humo.

Mara baada ya shughuli zote Meneja wa Shirika la Posta Mkoa wa Mwanza alifanya kikao na wafanyazi wote wa mkoa wa Mwanza na wilaya zake zote.

Sambamba na hilo, Mkoa unatarajiwa kuandaa tafrija fupi yenye lengo la kukuza mahusiano kwa wafanyakazi wa Shirika la Posta mkoani Mwanza huku Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) kanda ya ziwa Mhandisi. Francis Mihayo pamoja na wageni mashuhuri ambao ni wafanyakazi wastaafu akiwemo Mzee Nyanda aliyekua Meneja wa Shirika la Posta mkoa wa Mwanza.




# 09 SHIRIKA LA POSTA YAENDELEA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI

Shirika la Posta Tanzania (TPC) limeendelea kuboresha utoaji huduma kwa wateja wake kwa kuongeza vitendea kazi Ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji.

Hayo yameonekana mara baada ya Mameneja Wakuu wa Shirika la Posta Bw. Constantine Kasese pamoja na Bw. Samwel Aron kuendelea kukabidhi magari kwa niaba ya Postamasta Mkuu Bw. Macrice Mbodo, ikiwa ni mwendelezo wa zoezi la kukabidhi magari kwa Mikoa ya kiposta nchini, lengo ni kuboresha huduma za usambazaji na usafirishaji nchini

Mikoa ambayo tayari imeshakabidhiwa vitendea kazi hivyo ni pamoja na Morogoro, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro na Mzizima.

Kuongezeka kwa vitendea kazi ikiwemo magari mapya, vifaa na hata rasilimali watu kutaboresha ufanisi wa kazi na wateja watahudumiwa kwa wakati, ufanisi na Shirika limewataka madereva watakaokabidhiwa magari hayo kuyatunza ili yalete tija kwa Shirika na wananchi kwa upana wake.

Shirika la Posta limekuwa na mchango katika sekta ya usafirishaji baada ya maboresho yaliyofanywa ikiwemo kufungua huduma za duka mtandao, vituo vya Huduma ya Pamoja na kununua magari mapya yanayofanya kazi masaa 24 kusafirisha mizigo katika mikoa yote Tanzania.




Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara wa Shirika la Posta Constantine Kasese akipeana mkono na Meneja wa Posta Mkoa wa Morogoro kama ishara ya kukabidhi gari katika mkoa. Wanaotazama ni watendaji wa Shirika la Posta Mkoa wa Morogoro




Kaimu Meneja Mkuu Rasilimali za Shirika la Posta Aron Samwel (wa nne kulia) akikabidhi gari kama kitendea kazi kwa Shirika la Posta mkoa wa Kilimanjaro



Posta
Let's Go!

# TANZANIA POSTS CORPORATION


Head Office: Posta House 12th Floor, 7 Ghana Street.
P.O.Box 9551, 11300 Dar es Salaam, Tanzania.
Fax: (022) 2113081 Mobile: (022) 2113394/ 2111715/2118280

Phone: +255 738 070 072
Email: pmg@posta.co.tz
Website: www.posta.co.tz


@posta_tz